

**Swali:** Kwanini Mungu alimkataa Mfalme Sauli na tunapata funzo gani?

---

**Jibu:** Sauli alikataliwa na Mungu kwasababu ya mambo makuu mawili,  
**1) UASI na 2) UKAIDI WA MOYO.**

Hayo ndio mambo mawili yaliyomkosesha Sauli, na biblia imeweka wazi..

*1Samweli 15:22 “Naye Samweli akasema, je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu Sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu.*

*23 Kwani KUASI ni kama dhambi ya uchawi, Na UKAIDI ni kama ukafiri na vinyago; Kwa kuwa umelikataa neno la Bwana, Yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme”.*

## **1. KUASI**

Kuasi maana yake ni kuondoka katika njia sahihi na kuwa adui wa hiyo njia. Ndicho kilichomtokea Sauli, Moyo wake ulianza kuondoka kwa MUNGU kidogo kidogo, na akaanza KWENDA KINYUME na sheria ya MUNGU huku akijua kabisa kuwa anachokifanya si sawa.

## 2. UKAIDI

Dhambi ya pili ya Sauli ni **“Ukaidi”**. Mkaidi ni mtu asiyeshaurika wala hakubali kubadili mawazo yake...anachokiamini amekiamini!!,...anachokishikilia amekishikilia!..

Na Mfalme Sauli alikuwa mkaidi kwa BWANA!, Kwani utaona alipofanya kosa la kwanza la kutoa dhabihu kinyume na sheria ya Mungu katika *1Samweli 13:18* na kukemewa na Bwana, lakini utaona anakuja kurudia kosa linalofanana na hilo katika *1Samweli 15:14* pale alipoleta dhabihu haramu kutoka kwa waamaleki na kutaka kuzitoa kwa Bwana.

Alileta kondoo na Ng’ombe (*walionona*) kutoka Taifa la Amaleki, ili amtolee Mungu dhabihu... Kwa jicho la Haraka inaweza kuonekana kuwa alifanya jambo la busara...lakini kwa jicho la ndani SAULI alifanya machukizo makubwa sana.

Kwani kitendo cha kutwaa Ng’ombe za watu wanaoabudu miungu,

ambao wanaitolea miungu yao, na tena hajui hizo ng'ombe zina historia gani..na kuzichukua hizo kisa tu zimenona kisha kumtolea Mungu, ilikuwa ni kitendo cha dharau kubwa sana (1Samweli 15:14-15)!!.. Ni sawa tu na kutwaa msharaha wa kahaba na kumletea Bwana ule alioukataza katika *Kumbukumbu 23:18*..

*Kumbukumbu 23:18 "Usilete ujira wa kahaba, wala mshahara wa mbwa, katika nyumba ya Bwana, Mungu wako, kwa ajili ya nadhiri yo yote; kwani haya ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako, yote mawili".*

Hivyo Sauli alikuwa mkaidi kwa Mungu.. kwani sheria inasema Usimchinjie Bwana Ng'ombe wala kondoo aliye na kilema au **MWENYE NENO OVU!** (*Kumbukumbu 17:1*)..Na hapa Sauli analeta Ng'ombe walionona lakini waliojaa maovu ya Waamaleki kama sadaka kwa Bwana. (*1Samweli 15:14-15*)!!.. Huo ni **UKAIDI MKUU**..

Na hata leo, Mambo haya mawili (**UASI na UKAIDI**) yanamchukiza Mungu.

*Yeremia 5:22 “Je! Hamniogopi mimi? Asema Bwana; hamtatetemeka mbele za uso wangu; mimi niliyeweka mchanga kuwa mpaka wa bahari, kwa amri ya daima, isiweze kuupita? Mawimbi yake yajapoumuka-umuka, hayawezi kushinda nguvu; yajapovuma sana, hayawezi kuupita.*

*23 Lakini watu hawa wana moyo wa KUASI NA UKAIDI; wameasi, wamekwenda zao.*

*24 Wala hawasemi mioyoni mwao, Basi, na tumche Bwana, Mungu wetu, aletaye mvua, mvua ya mwaka, na mvua ya vuli, kwa wakati wake; na kutuwekea juma za mavuno zilizoamriwa.*

*25 Maovu yenu yameyageuza haya, na dhambi zenu zimewazuilia mema msiyapate”.*

Maran atha!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

### **Mafundisho mengine:**

**ROHO MBAYA KUTOKA KWA BWANA.**

**DHABIHU ZA ROHO NI ZIPI? (1Petro 2:5)**

**Dhabihu ni nini?**

**Gudulia ni nini? (1Samweli 26:11).**

**Habari ile ya Pilato kuchanganya zile damu za wayahudi na pamoja na dhabihu zao,(Luka 13) ilihusu nini?**

**Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp